MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 8 TOLEO 31

MACHI 18, 2009

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

SAKATA LISILOKWISHA

PORTEK: DOWANS GANI?



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Na. Fred Katunzi



Kampuni ya Dowans Tanzania Limited inayomilikiwa na mfanyabiashara mkubwa wa Oman na Falme za Kiarabu Brig. Gen Suleiman Mohammed Yahya Al-Adawi ilijipa ujiko isiyokuwa nao na kutangaza kuwa wanahisa wake wakubwa ni makampuni mawili ya kigeni ya Dowans Holdings ya Costa Rica (Marekani ya Kusini) na ile ya Portek ya Indonesia. Uchunguzi wa kina wa Cheche umeweza kuthibitisha pasipo shaka lolote kuwa kampuni ya Portek ya Indonesia ambayo inatajwa katika nyaraka za BRELA haina hisa yoyote wala kutambua hisa zinazotajwa kuwemo kwenye kampuni ya Dowans Tanzania Limited.



Mawinchi yaliyoletwa na kampuni ya Portek Bandarini Dar

Kwa mujibu wa habari mbalimbali ambazo zimekuwa zikirudiwa na vyombo vyetu vya habari kampuni ya Portek ya Indonesia ndiyo mwekezaji kwenye Dowans Tanzania Limited. Kwa mujibu wa makala moja iliyoandikwa na mmoja wa waandihi mahiri nchini miaka karibu miwili iliyopita kampuni ya Portek ina asilimia 39 wakati kampuni ya Dowans Holdings ya Uarabuni ina asilimia 61.

Ili kuhakikisha kuwa tunazungumzia kampuni hiyo hiyo nakala za BRELA **(inaendelea Uk. 2)**

MWAKYEMBE KUJIBU *MTANZANIA* LEO

Na. Mwandishi Wetu

Mbunge wa Kyela Mhe. Dr. Harrison Mwakyembe kesho asubuhi anatarajiwa kuzungumza na waandishi wa habari jijini Dar-es-Salaam katika kile kinachotarajiwa kujibu madai yaliyotolewa kwenye gazeti la Mtanzania la Jumatatu tarehe 15 Machi ambapo alidaiwa kuwa anaumiliki wa kampuni ya kufua umeme na ya kuwa hakutangaza maslahi hayo wakati anaongoza Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchungwa kampuni ya kuzalisha umeme ya Richmond.

Kwa mujibu wa gazeti la Mtanzania "Wachunguzi wa mambo wanaamini kuwa ushujaa wa Dk. Mwakyembe kuishambulia kampuni ya Richmond, na baadaye Dowans, unatokana na mgongano wa kimaslahi.

Katika taarifa **(inaendelea Uk. 2)**

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimerushusiwa!**

Ndani ya Toleo Hili

Portek: Dowan nani?	1,2
Mwakyembe ajibu	1,2
Portek: Dowans nani?	3,4
Maoni ya Mhariri	4
Nguvu ya Hoja	4,5
Da'Jessy: na "Umodo"?	5
Picha, Katuni na Maoni	6

PORTEK NA DOWANS

zinaonesha kuwa anuani ya kampuni hiyo ya Portek ni PORTEK SYSTEMS AND EQUIPEMENT LIMITED
20 HARBOUR DRIVE #02-01 PSA VISTA SINGAPORE 117 612. Anuani hiyo ni kweli ni ya kampuni tanzu ya yenye jina hilo ambayo kampuni yake mama inaitwa Portek International.

Kuwa kampuni ya Portek ya Indonesia yenye anuani hiyo hapo juu ndiyo mwekezaji wa kwenye Dowans haina utata kwani hilo liliwahi kuandikwa na mojawapo ya magazeti mashuhuri nchini tena na mwandishi makini. Uchunguzi wetu unaonesha kuwa wakati kampuni ya Dowans ilipoingia nchini gazeti moja linalomilikiwa na Mbunge wa Igunga Mhe. Rostam Aziz ambaye ndiye aliyetoa mwaliko kwa Bw. Al-Adawi kuingia nchini liliandika kuhusu makampuni mawili yaliyona hisa kwenye kampuni ya Dowans Tanzania Limited.

Vyanzo vyetu vya kuaminika kabisa vimedai kuwa mwandishi wa makala hiyo ya kuipamba Dowans alikuwa mwandishi wa habari wa siku nyingi nchini ambaye alikuwa mwajiriwa wa Bw. Rostam na ambaye sasa amepata wadhifa Ikulu. Katika makala yake hiyo mwandishi huyo aliandika ifuatavyo kuhusu kampuni ya Portek yenye hisa kwenye DTL:

" Nayo nguvu ya kampuni ya Portek inafanya biashara ya ***uzalishaji wa umeme****, uandisi wa umeme, uandisi wa gesi na mafuta, na uandisi wa jumla, Kampuni hiyo imeorodheshwa katika Soko la Mitaji la Singapore na ina shughuli katika nchi nyingi duniani zikiwamo Singapore yenyewe, Australia, UAE, China, Algeria, Indonesia, Uingereza, Pakistan, Korea Kusini, Taiwan, Marekani, Peru, Malaysia, Luxembourg na Italia.*

Kwa pamoja Portek na Dowans zimeshiriki kuendesha miradi ya pamoja katika nishati, kuendesha bandari, kuzalisha umeme, na kushirikiana katika biashara ya kukodisha mitambo mikubwa ya ujenzi na shughuli nyingine." (msisitizo wetu)

Bahati mbaya uchunguzi wa Cheche umeonesha pasipo shaka kuwa kampuni ya Portek haijihusishi na mamnbo ya uzalishaji umeme mahali popote duniani. Kwa mujibu wa kampuni hiyo shughuli zake zote zinazunguka katika shughuli za mambo ya bandarini, na hasa katika suala la kuleta teknolojia ya kisasa katika matumizi ya kuhamisha mizigo bandarini. Jina la kampuni hiyo lingeweza kuwa ishara tangu mwanzo "Portek" yaani "Port Technology". Kuna kampuni nyingine ya vyuma ya Marekani inayotumia jina la "Portec" na nyingine inayotengeneza mikanda ya mashine mbalimbali.na bila ya yashaka sababu pia ya kutafautisha majina.

Tovuti ya kampuni hiyo inasema hivi kuhusu shughuli zake "The Portek Group, established in 1988 and headquartered in Singapore, has emerged as a global specialist provider of solutions to the port industry. We are able to deliver both capacity and productivity to port operators by enabling them to gear up and streamline their operations over a relatively short period of time. Portek's range of competencies includes turnkey engineering solutions such as port equipment modernisation, modification and maintenance, equipment leasing and sale, and distribu-

MWAKYEMBE KUJIBU GAZETI LA MTANZANIA

hiyo gazeti hilo ambalo linatajwa umilikiwa na Mbunge wa Igunga ambaye alihusika katika kuikaribisha kampuni ya Dowans nchini Mhe. Rostam Aziz "Dk. Mwakyembe na wenzake walianzisha kampuni yao kabla ya ujio wa kampuni iliyozua utata mkubwa wa Richmond. Matarajio yao yalikuwa kwamba wazalishe umeme na kisha waiuzie Tanesco, lakini ujio wa Richmond ulionekana kutaka kuwakwaza. Richmond ilisababisha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Lowassa, ajiuzulu Februari mwaka jana."

Kutokana na madai hayo na mengine mengi yaliyomo kwenye taarifa ya gazeti hilo, vyanzo vya karibu vya Dr. Mwakyembe (Pichani) vimeiambia KLHN kuwa Dr. Mwakyembe atatoa maelezo yake na vinasema kuwa "mstari uliokuwa hauvukwi kesho utavukwa".

Mmoja wa watu wa karibu wa Mwakyembe wameiambia KLHN kuwa "Dokta atawatolea uvivu kesho". Alipobanwa kuelezea ni kwa jinsi gani uvivu huo utatolewa jamaa huyo alikataa na kusema "subirini kesho". Hadi tunakwenda mitam-



boni jioni hii haijawekwa sawa mkutano huo utafanyika wapi lakini muda uliopangwa hadi hivi sasa ni saa nne za asubuhi.

Mjadala wa kuhusu Dr. Mwakyembe umeibua gumzo kubwa kwenye mtandao na mitaani ambapo watu mbalimbali wameonesha kuamini taarifa za awali huku baadhi yao wakimtaka ajiuzulu kutokana na "mgongano huo wa maslahi"

Hata hivyo sauti chache zimetoa wito wa kutaka watu wasubihri kusikia majibu na maelezo ya Bw. Mwakyembe kuhusu madai hayo.

Wapo wanaomini kuwa kwa namna fulani kama ni kweli Dr. Mwakyembe hakutangaza maslahi yake yawezekana amejiweka kwenye nafasi ngumu. Wengine hata hivyo wanaamini kuwa maelezo ya Dr. Mwakyembe baadaye leo yatakata ule "mzizi wa fitina".

Ripoti ya Kamati Teule ya Bunge ilitoa wito kwa Waziri Mkuu kupima kuhusika kwa ofisi yake na yeye mwenyewe katika suala la Richmond na kuamua kuchukua hatua zinazopasa. Aliyekuwa Waziri Mkuu baada ya kupima tuhuma dhidi yake na ofisi yake aliamua kujiuzulu nafasi yake na kusababisha baraza la Mawaziri kuvunjika.

Tangu wakati huo kuna kila dalili kuwa Bunge la Muungano limegawanyika kati ya kambi ya "Lowassa" na kambi ya "Mwakyembe". Kambi hizi mbili zimekuwa zikirushiana madongo kila wanapopoata nafasi. Ni wazi kuwa leo tena tunaweza kushuhudia hoja nzito zaidi ambazo zinaweza kabisa kuvuka mipaka na kuleta mgongano wa kambi hizi katika mahakama zetu. Yetu macho.

KARIBU MWANAKIJIJI.


PORTEK NA DOWANS

tion of components and parts."

Yaani, "Kampuni ya Portek, iliyoanzishwa mwaka 1988 na yenye makao makuu huko Singapore imeibuka kuwa ni kinara katika kuleta utatuzi wa shughuli mbalimbali za bandarini. Tunaweza kuwapatia yote mawili yaani uwezo na uzalishaji mzuri wale wanaoendesha bandari kwa kuwawezesha kuboresha na kurahisisha utendaji wao ndani ya muda mfupi. Kati ya mambo ambayo Portek inaweza kufanya ni pamoja na miradi ya kujenga na kukodisha kama vile kupyaisha vifaa mbalimbali, kurekebisha na kutengeneza, kukodisha vifaa na kuuza, kusambaza vifaa vya ndani vya mashine na vipuri."

Katika maelezo yake hakuna mahali popote panapoonesha kuwa kampuni hii inahusiana na nishati. Cha kushangaza zaidi ni kuwa katika makala hiyo mwandishi aliripoti ifuatavyo "Kwa pamoja Portek na Dowans zimeshiriki kuendesha miradi ya pamoja katika nishati, kuendesha bandari, kuzalisha umeme, na kushirikiana katika biashara ya kukodisha mitambo mikubwa ya ujenzi na shughuli nyingine." Hata hivyo hakuna mfano wa mahali popote duniani ambapo makampuni hayo yamewahi kufanya mradi wowote.

Katika kuhakikisha kama kampuni ya Portek inahisa zozote katika Dowans, tumepata nakala za ripoti zake za kifedha za mwaka 2006, 2007, na 2008. Katika ripoti hizo ambazo zinatakiwa ziwe na taarifa zote za kampuni kuhusu mapato yake, shughuli



Kielelezo 1

zake, madeni n.k Jina la kampuni ya Dowans Tanzania Limited halionekani.

Kwa mwaka wa 2007 na 2008 kampuni ya Portek Systems and Equipment Ltd ambayo ndiyo tumeambiwa imewekeza kwenye Dowans chini yake yapo makampuni machache tu na kutoka Afrika iko kampuni moja tu ambayo wao wana hisa, na kampuni hiyo iko Algeria.

Ukiangalia kielelezo 1 cha mwaka 2007 kampuni ya Portek Systems and Equipment Ltd ilikuwa na makampuni 5 chini yake na kiasi cha hisa pia kinaweza kuonekana. Dowans Tanzania Limited haipo! Ripoti yao ya mwaka 2008 nayo (kielelezo 2) nayo ni hivyo hivyo inaorodhesha makampuni yaliyokuwa chini ya PSE Ltd kwa mwaka huo pamoja na hisa zake, ni yale yale 5.

Katika uchunguzi wetu tulijaribu kufuatilia ni kwanini wajanja walitumia jina la kampuni hiyo kubwa na kuliweka katika Dowans Tanzania Limited? Uchunguzi wetu unaonesha kuwa kati ya mwaka 2006 na 2008 kampuni ya Portek ilisafarisha mitambo (cranes) za kutumika katika bandari ya Dar (kitu ambacho ni kazi yao).

Mwaka 2008 ilisafarisha mawinchi ya kawaida kutoka Indonesia kuja Tanzania na mwaka 2007 pia iliileta mawinchi makubwa 2 kuja bandari ya Dar-Es-Salaam. Uchunguzi wetu unaonesha kuwa mawinchi hayo yanatumiwa leo hii na kampuni ya kupakua mizigo ya TICTS. Mmoja wa wamiliki wa kampuni hiyo ambaye alitimuliwa na Bodi yake ni aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini Bw. Nazir Karamagi.

Katika kuhakikisha habari za wachunguzi wetu tuliwasiliana na mmoja wa maafisa wa shirika la Portek huko Indonesia na kumuuliza kuhusu umiliki wa kampuni yake naye alionesha kushangazwa na habari hiyo kwani alisema wazi kabisa kuwa kampuni yao haijawekeza kwenye uzalishaji umeme mahali popote kwani kufanya hivyo itakuwaa ni nje ya majukumu ya familiar ya mmiliki wa kampuni hiyo.

Mtindo huu wa wawekezaji kuja nchini huku wamebeba majina makubwa ndiyo ulitumiwa pia na kampuni ya Richmond ambayo kwa mujibu wa ripoti ya Kamati Teule ya Bunge. Katika taarifa yake iliyosomwa na mwenyekiti wake Dr. Harrison


Soma bure

HOJA YA MWANAKIJIJI:TUTATOKA KWELI HAPA?

Mwakyembe kamati hiyo ilidokeza kuwa "viongozi wote wa Serikali waliohojiwa na Kamati Teule walisisitiza kuwa uamuzi wa kuipa Richmond Development Company LLC kazi hiyo ya kuzalisha umeme wa dharura, ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na madai ya kampuni hiyo kuwa na ubia na kampuni maarufu ya Pratt & Whitney."

Hivyo watu wale wale waliojua kuwa ukija na jina kubwa unapapatikiwa wakaamua kujibambikiza ubia na kampuni ya Portek na kuipa "hisa" na wakajua wakiipamba vizuri basi Watanzania watakubali tu. Tunaamini kuwa kuingia kwa Dowans kuliingia kwa ulaghai (under false pretence) na ya kuwa hawakuingia wakiwa na nia ya kuaminiana (good faith). Yote haya mawili yanatosha kabisa kuilazimisha serikali kuitaifisha mitambo ya Dowans na kuanza kuitumia bila kulazimika kulipa chochote!

Tunaamini mwizi akiingia ndani ya nyumba yako kuiba na wakati ameingia akaangusha jiwe la almasi, kwenye



nyumba yako. Basi mwizi huyo ukimtumia una haki ya kutaifisha jiwe hilo! Hapa ndipo sera ya kweli ya utaifishaji inapotakiwa kutumika. Tusiache mitambo ya Dowans iondoke (tunatoa wito ulinzi uwekwe hata wa wananchi wenyewe!) na tusikubali kuinunua, bali tuitaifishe.

Tutakubali kuwaachia majenereta hayo pale tu watakapokuja Portek Systems and Equipment Ltd kutuonesha kuwa ina hisa yoyote kwenye kampuni ya Dowans Tanzania Limited ukiondoa kwenye makaratasi ya BRELA.

Vinginevyo tunatajia Uamuzi wa kutoizawadia Dowans utasimama bila kujali mtu au kumuogopa mtu.

MAONI YA MHARIRI

Kama tulivyodokeza wiki iliyopita wiki hizi mbili zitakuwa ni wiki mbili za mwisho za kupokea wanachama wapya ambao wamejiandikisha kupokea kijarida hiki kwa njia ya mtandao.

Lengo letu toka mwanzo ilikuwa ni kuwa na waliojiandikisha wapatao

SWALI LA WIKI:

Serikali kupitia Waziri wa Nishati na Madini Mhe. William Ngeleja imetaka wananchi tusitishe mjadala wa Dowans. Imetutaka tuufunge mjadala huo. Je unakubaliana na wito huo kwamba haya ya Dowans tuwaachie tu serikali wafikie maamuzi bila kufanya sauti zetu nasi zisikike?

majibu yako: **mhariri@klhnews.com**

1000 tu ambao itakuw rahisi kwetu kuwasiliana nao na kubadilishana mawazo na mijadala mbalimbali.

Lengo letu kama tulivyoanisha kwenye ripoti ya mwaka ya tovuti yetu ya mwanakijiji.com (unaweza kupata nakala yako pale) ni mwaka huu kutoka kulalamika na kuelekea kuhamasika. Ili tuweze kufikia lengo hilo tunataka tuwe na mahali pa kuweza kukusanya uwezo, elimu na vipaji vyetu kuanza kuibadili nchi yetu kuifanya vile tunavyotaka au tamani iwe.

Katika hili hatuzungumzii suala la kisiasa bali masuala ya kijamii na kujitolea. Tuna uhakika wapo Watanzania wengi ambao wanasubiri nafasi au uratibu wa kitu cha kufanya ili na wao watoe mchango ambao wamekuwa wakiutamani.

Hivyo, sisi tunaamini kabisa kuwa tuna nafasi ya pekee na nzuri ya kuchochea mabadiliko hayo ya kifikra kwani mpango upo tayari na kwa miaka mitatu tumeweza kuongoza mjadala huu wa mabadiliko ya kifikra.

Tunachosema ni kuwa zimebaki nafasi chache tu kwa mtu yeyote anayetaka kujiunga nasi kufanya hivyo na baada ya hapo tutakuwwa tunaendelea kupeana taarifa ya nini tunafanya na kubadilishana mawazo tufanyeje kitu hicho.

Jiunge nasi kwa kuniandikia barua pepe kwa anuani ya **mhariri@klhnews.com** na tutafurahi kwa wewe kuwa mmoja wetu.

Soma Bure
hoja zenye nguvu

STENDI YA UBUNGO: HADI WAZIRI MKUU AJE?

Na. M. M. Mwanakijiji

Nimebakia natikisa kichwa baada ya kusoma na kufuatilia Wizara ya Waziri Mkuu jijini Dar wiki iliyopita. Kilichonishangaza ni maagizo ambayo yametolewa na ripoti ambazo ziliandikwa kuhusu ziara yake hasa linapokuja sualala kukusanya mapato kwenye stendi ya mabasi ya pale Ubungo.

Katika ziara yake kwenye eneo hilo maarufu ambalo kwa wengi ndiyo mlango wao wa kuliingia jiji hilo la Kandoro Waziri Mkuu alitoa wito kwa Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali kufuatilia kituo hicho kuona suala zima la mapato likoje.

Kituo cha Mabasi cha Ubungo hakina bodi inayosimamia wala Kamati lakini inadaiwa kimeweza kuingia mkataba na kampuni ya ukusanyaji mapato ambayo hutoa kikasi cha shilingi milioni moja na nusu kwa Halmashauri ya Jiji.

Kampuni inayosimamia mradi huo inamilikiwa na na mtoto wa kiongozi wa zamani nchini na Mbunge wa kuteuliwa Mhe. Kingunge Ngombale Mwiru aitwaye Kinjekitile (Pichani).

Kuanzia kwa kuingia kwa kampuni hiyo katika mradi huo kumekuwa na lawama na tetesi za ufisadi uliosababisha kampuni hiyo kupewa tenda hiyo kwa kile kinachodaiwa kubebwa na watu mbalimbali.



Cha kushangaza ni kuwa kwa muda wote huu inajulikana kuwa mahali hapo hakuna bodi wala utawala unaoeleweka; inajulikana kuwa kiasi ambacho wamekubaliana ukilinganisha na magari yanayoingia hapo ni kidogo mno, inakuwaje kampuni hiyo ikaendelea kufanya shughuli zake?

NI wazi kuwa kuna watu waoga kwenye Halmashauri ambao wameshindwa kusimamia maslahi ya watu wa Dar na taifa. Watu hawa ambao walitakiwa kuweka maslahi ya taifa mbele ni dalili tu ya ubovu tulio nao kwenye masuala ya mikataba.

Hivi kweli watu hawa wanaweza vipi kuendelea na kazi zao kama kawaida? Bila ya shaka wanafanya hivyo kwa sababu hakuna tishio la matokeo mabaya kwao. Kwani ni nani anayekosa fedha hizo?

Kwao wao hawa serikali ikipoteza fedha siyo tatizo. Mawazo ya namna hii tunayakuta katika miradi yetu mingi tu kiasi kwamba tumefikia mahali pa kuona kuwa fedha za umma zikichotwa na kutoweka ni jambo la kawaida tu.

Sasa tumefikia hadi Waziri Mkuu na msafara wake aje na kuwaambia watu na akili zao na wengine wanaitwa wasomi kuwa "hili siyo sahihi".

Angalia maneno ya Waziri Mkuu "Mimi sijui ni nani anayemiliki ile kampuni, lakini hapa ninachokizungumzia kinahusu maslahi ya umma. Tuone hicho kinachofanyika huko ni kwa maslahi ya nani?" Kwamba hata Waziri Mkuu ameshindwa kutaja jina la mmiliki wa kampuni hiyo!

Kama wao wenyewe wanaogopana hivyo wananchi wakaida itakuwaje?

Hata hivyo ni lazima tukubali kuwa angalau sauti za manung'uniko ambayo yamekuwepo kwa muda mrefu zimeanza kupata msikilizaji. Sijui ni kwa kiasi gani CAG atafuatilia (kwani sioni sheria inayompa Waziri Mkuu madaraka ya kumuagiza CAG kufanya jambo lolote).

Lakini tusipoangalia tutajikuta tunamsubiri Waziri Mkuu au Rais kuja kutuambia kitu ambacho tayari tunakijua halafu tukabakia kushangalia kuwa Waziri Mkuu kasema. Tunaweza kujikuta Waziri Mkuu anakuja kutuambia kile ambacho tangu tukiwa watoto tulikuwa tunajua tunapaswa!

DA' JESSY: UNAPOMPIGA ALIYEMPIGA RAIS MSTAAFU!

Na. Jessica L Fundi

Mtu mnafiki ni vigumu sana kujijua. Mnafiki ni mtu ambaye wakati mwingine anafanya kitu ambacho anamkataza mwingine kufanya.

Kama Watanzania wengine nilishtushwa, kusikitishwa na kuchukizwa na kitendo cha kijana mmoja wiki iliyopita wakati wa siku kuu ya maulidi alipoamua kumchapa kibao Rais Mstaafu katika hafla ya Maulidi.

Wapo watu ambao wamejaribu kutolea mawazo kitendo hicho cha kishenzi huku wengine wakijaribu kuhalalisha kuwa ni suala la kidini.

Hata hivyo ukweli unabakia kuwa katika Tanzania sheria haiwezi kamwe kuchukuliwa na mtu kwa kisingizio cha dini. Kama kila mwenye dini yake na imani yake akiruhusiwa kumchapa vibao au fimbo mtu anayesema kitu au kufanya kitu kinyume cha mafundisho ya dini hiyo basi humu nchini itakuwa mshike mshike.



Naweza kuwa peke yangu nikilaani kitendo cha waumini ambao walijiona wao ni bora zaidi walipoamua kumpiga magumi na mateke na magazeti mengine kuandika ati "yalimuadhibu" kijana huyo wakati alikuwa tayari mikononi mwao, hakuwa na uwezo wa kukimbia na kulikuwa na maafisa wa Polisi karibu!

Sijasikia mtu akitaka watu hawa wachukuliwe hatua vile vile kwani picha zao zipo na mikanda ya video ipo. Kama waumini hawa waliona kuwa kitendo cha kumpiga Rais ni kibovu na hakifai mbele ya jamii kwanini walifikiri cha kwao cha kumpiga mtuhumiwa kinakubalika?

Tunaposema kuna haki za binadamu, hatumaanishi "haki za viongozi" au "haki za wenye madaraka". Tunaposema haki za binadamu tunamaana haki za uzao wote wa Adam na Hawa! Maana yake, Rais Mwinyi hana haki zaidi za binadamu kuliko Mmachinga au Tajiri fulani kuwa ana haki zaidi kuliko masikini "yule".

Tukitambua hili tutaona kuwa kama wakubwa waliotuchapa vibao kwa kuiba mabilioni wanafikishwa mahakamani kwa heshima zote na wezi wa kuku (kama ilivyotokea Moshi wiki hii) wanauawa papo kwa papo ina maana kuwa sisi ni Taifa la wanafiki, tumegeuza vipaumbele na dhana nzima ya haki za binadamu imetupita kushoto!

Email: dajessy@klhnews.com

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha ya Wiki



Kijana aliyemzaba Mzee Mwinyi akipigwa na yeye

PATA HABARI MOTOMOTO NA MIJADALA

http://www.mwanakijiji.com

Jiandikishe kushiriki mijadala, kupata habari, kusikiliza muziki masaa 24 na matangazo ya moja kwa moja kila mwishoni mwa juma.

Ukizungumzia habari, unatuzungumzia

KATUNI ZA WIKI





KUTOKA KWENYE MTANDAO

Ni nani kwenye safu ya uongozi Tanzania asiye fisadi? Maana karibu kila kukicha kuna tuhuma za mafisadi wapya.—**Nyani Ngabu**

Tutahakikisha Rais Kikwete anatueleza wamiliki wa Kagoda na wezi wetu wengine ni kinanani kwani mabilioni ya fedha yamechotwa na hatua hazichukuliwi huku wengine wakijulikana wazi...umaskini wa nchi hii unatokana na viongozi wetu kupenda ubabena kuamini watakaa madarakani milele. –**Freeman Mbowe**

Sio kweli kwamba hakukuwa na ulinzi, lakini yawezekena walijisahau kwa sababu Mzee Mwinyi alikuwa katika eneo la usalama wa kutosha, na ni eneo la ibada ambapo hakuna aliyetegemea kuwa tukio hilo lingetokea— Waziri **Sophia Simba**

Tuliapa kuilinda Katiba ya nchi hii, hivyo hakuna tutakayemwogopa katika kutekeleza kazi ila Mwenyezi Mungu tu—**VP Shein**

Hakuna ufisadi bwana, yule Mkurugenzi alijichanganya tu katika kutoa maelezo, makusanyo ambayo si ya mlangoni mimi niliacha Sh milioni 61 kwa mwezi, lakini siku hizi nasikia ni milioni 80 kwa mwezi—**Mukama**

Hivi ni uzuri gani au ufanisi upi mkubwa uliomfanya JK kukataa Dr Idrissa kujiuzuru pale alipotaka kufanya hivyo? je JK alikuwa aanajua kuwa akija mtu mwingine pale TANESCO watashindwa kupanga hivi wanavyopanga leo? Idrissa na scandal ya Rada bado Rais wetu anamwamini kiasi hicho Idrissa kuja na kututisha kichwa mchungwa? sawa lakini mungu si Athumani! - **Kite Munganga**

Hawa watu wanaojiita viongozi wetu inabidi wakae chini waaanze kudesa upya maana naona sometimes si kwamba wanafanya makusudi,bali hawajui hata la kufanya . Kwa hiyo wao ni kuhamisha na kukariri tu. Wakiulizwa nini kimechangia umasikini hawajui
—**Jmushi 1**

TOA NAKALA MOJA

Cheche za Fikra

Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie:
mhariri@ klhnews.com

Tovuti: http://www.mwanakijiji.com

***Kanusho:** Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.*